

# wakulima na wafugaji

uimarishaji wa mahusiano



SUA Project

Warsha ya Tatu ya
Wakulima wa Kanda ya
Nyanda za Juu Kusini
Kuhusu

# Mahusiano Baina ya Wakulima na Wafugaji

Iliyofanyika Mjini Songea
Tarehe 26 – 29 Novemba 2001

Warsha hii ilitayarishwa na

Kamati ya Utekelezaji ya
Mradi wa
**Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa**
**Wakulima Wadogowadogo Tanzania:**
Mradi wa Utafiti Unaotilia Mkazo Wanawake

Mradi huu upo chini ya

Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili

(TARP II – SUA Project)

***Imetayarishwa na***

A. M. Bakari

***Na Kuhaririwa na***

Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B Kinabo | Mratibu |
| Dk. (Bi.) J. Lyimo Macha | Mjumbe |
| Prof. R.E. Malimbwi | Mjumbe |
| Prof. E.K. Batamuzi | Mjumbe |
| Prof. A.J. Tarimo | Mjumbe |
| Dr. P.J. Makungu | Mjumbe |

**ISBN: 9987 605 56 7**

***Kimechapishwa na:***

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo namba: TS 2-34

© TARP II – SUA Project 2002

# YALIYOMO

**Dibaji** ........ v
**Vifupisho** ........ vii
**Muhtasari** ........ ix

1. **UTANGULIZI** ........ 1

**1.1 Maandalizi** ........ 1

**1.2 Madhumuni** ........ 1

**1.3 Utambulisho na ufunguzi** ........ 2

2. **KUAINISHA MATATIZO CHANZO NA KIPAUMBELE KATIKA UTATUZI** ........ 3

**2.1 Kutathmini mahusiano baina ya wafugaji na wakulima wa mazao** ... 3

**2.2 Maelezo kuhusu mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo** ........ 5

**2.3 Kubainisha matatizo, jinsi yanavyohusiana na umuhimu wake katika kipaumbele** ........ 5

2.3.1 Matumizi ya rasilimali hasa ardhi na maji ........ 6

2.3.2 Utendaji wa viongozi na serikali ........ 9

2.3.3 Mahusiano ya kijamii ........ 12

**2.4 Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi** ........ 14

2.4.1 Kikundi cha wafugaji kutoka wilaya za Mbeya ........ 14

2.4.2 Wafugaji ........ 15

2.4.3 Wakulima wa Mpanda na Njombe ........ 16

2.4.4 Wafugaji wa Wilaya za Mbeya ........ 16

2.4.5 Washauri wa ugani na watafiti ........ 17

2.4.6 Wataalam waandamizi wa wilaya ........ 18

3. **MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI, MIKAKATI YAKE NA WAHUSIKA KATIKA UTEKELEZAJI** ........ 19

**3.1 Utatuzi wa rushwa** ........ 19

3.1.1 Ufumbuzi ........ 20

3.1.2 Mikakati ........ 20

3.1.3 Watekelezaji na wajibu wao ........ 20

**3.2 Utatuzi wa kuwezesha umilikaji na matumizi sahihi ya ardhi** 21

3.2.1 Ufumbuzi.............................................................. 21

3.2.2 Mikakati.............................................................. 22

3.2.3 Watekelezaji na wajibu wao.............................................. 22

**3.3 Elimu duni ya kilimo na ufugaji........................................** 23

3.3.1 Ufumbuzi .............................................................. 23

3.3.2 Mikakati.............................................................. 23

3.3.3 Watekelezaji na wajibu wao .............................................. 23

**4. HITIMISHO...................................................................** 23

**4.1 Tamko la warsha ...........................................................** 23

**4.2 Kufunga ....................................................................** 24

**VIAMBATANISHO** 25

Kiambatanisho Namba 1: Orodha ya Washiriki..................................... 25

Kiambatanisho Namba 2: Kielelezo cha mfano hai wa ajali nyingi barabarani.. 27

Kiambatanisho Namba 3: Michoro inayoonesha uhusiano wa matatizo, viini vyake, na kipaumbele katika utatuzi wa kila iini........ 28

# DIBAJI

Chapisho hili linawasilisha Mwenendo wa Warsha ya Tatu ya Wakulima wa Kanda ya Mashariki kuhusu uimarishaji wa mahusiano yaliyopo baina ya wakulima wa mazao na wafugaji. Warsha ilifanyika katika Kituo cha Don Bosco Mjini Songea tarehe 26 hadi 29 Novemba 2001.

Warsha hii ni moja ya warsha ambazo zimepangwa kufanyika kama shughuli muhimu za kuutekeleza mradi wa **Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania.** Mradi huu ambao ulianza rasmi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD), na unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo. Warsha hizi zina madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo na washika dau wengine ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo.
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo.
3. Kudadisi ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi.
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

Kamati ya Utekelezaji wa Mradi inatarajia kuwa chapisho hili litakuwa la manufaa kwa wadau mbalimbali, na mapendekezo yaliyotolewa na washiriki wa warsha yatachangia katika juhudi za kuimarisha uhakika wa chakula nchini.

*L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

*Novemba 2001*

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| NLH | Agricultural University of Norway (*Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo*) |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation (*Shirikia la Maendeleo la Norway)* |
| SUA | Sokoine University of Agriculture (*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo*) |
| TARP II | Tanzania Agricultural Research Project Phase Two ( *Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili*) |



*Washiriki wa warsha wakiwa kwenye picha ya pamoja*

# MUHTASARI

Warsha ilishirikisha wakulima wa mazao, wafugaji, wataalamu wa ugani, watafiti na watumishi waandamizi katika idara za kilimo, mifugo, ardhi na mipango kutoka wilaya za Iringa vijijini, Mbarali, Mpanda, Chunya, Njombe na Mbeya vijijini. Lengo kuu la warsha lilikuwa kutafakari vyanzo vya migogoro baina ya wafugaji na wakulima inayotokea katika wilaya hizo na hatimaye kubaini mbinu muafaka katika kuepuka migogoro hiyo na kupendekeza mikakati ya namna ya kuitatua.

Washiriki wa warsha waliridhika kuwa mahusiano baina ya wakulima wa mazao na wafugaji katika wilaya zao ni mabaya. Mahusiano mazuri pekee yaliyopo baina ya wakulima wa mazao na wafugaji ni katika kuuziana bidhaa.

Mazingira muhimu katika migogoro baina ya wafugaji na wakulima wa mazao katika wilaya hizo ni wafugaji wasio na asili ya kilimo cha mazao kuishi pamoja na wakulima wasio na asili ya ufugaji. Hata hivyo wafugaji wa jamii ya kimasai wanakabiliwa zaidi na migogoro baina yao na jamii za wakulima wa mazao ikilinganishwa na jamii zingine za wafugaji.

Kuingiliana katika matumizi ya ardhi na maji unaotokona na uwiano mbaya uliopo wa matumizi ya rasilimali hizo katika shughuli za ufugaji na kilimo cha mazao ni chanzo cha msingi cha migogoro. Vyanzo muhimu vya kutokuwepo kwa uwiano sahihi wa matumizi ya ardhi na maji ni:

- Kutokuwepo kwa mipango ya kitaifa ya matumizi ya ardhi na maji kwa uwiano sahihi katika ufugaji na kilimo cha mazao
- Serikali kugeuza maeneo kuwa hifadhi au kufungua miradi kwenye maeneo ya wakulima au malisho
- Utekelezaji mbaya wa mipango ya serikali au mipango hiyo kutotekelezeka kutokana na kuhitajika rasilimali kubwa ambazo huwa vigumu kupatikana.
- Sheria dhaifu na zisizosimamiwa kikamilifu juu ya udhibiti wa matumizi bora ya rasilimali. Vyombo vya dola hutumia mwanya wa udhaifu wa sheria zilizopo, vyombo vya haki vya kata kutojua sheria na uelewa mdogo wa haki walionao wafugaji na wakulima kupoteza haki ya waathirika wa migogoro hali ambayo inatafsiriwa kuwa ni kukithiri kwa rushwa miongoni mwa watendaji wa serikali. Hali hiyo imepelekea waathirika wa migogoro kukatishwa tamaa na utendaji wa vyombo vya dola na kujichukulia sheria mikononi mwao.

Tofauti kubwa ya mila na desturi iliyopo baina ya wafugaji na wakulima wa mazao katika maeneo yenye migogoro imesababisha kudharauliana kijamiii na kiuchumi na hivyo kujenga chuki miongoni mwa jamii. Chuki hiyo imeondoa uwezekano wa kusuluhisha kijamii migogoro baina yao. Desturi ya wafugaji kupenda sifa huwa kichocheo cha kufuga mifugo mingi kuzidi uwezo wa eneo husika. Aidha, wakulima wa mazao kwa upande wao hujiona kuwa na haki zaidi ya kumiliki ardhi yote bila kujali mahitaji ya watumiaji wengine.

Mbinu hafifu katika kilimo cha mazao na ufugaji kutokana na elimu duni ya kilimo na ufugaji pia huchangia katika kutokuwa na uwiano mzuri wa matumizi ya ardhi na maji.

Aidha wakulima na wafugaji walionekana kutotumia utaalamu katika shughuli zao kutokana na kuwepo teknologia zisizotekelezeka kwa urahisi, zinazohitaji gharama kubwa na mafunzo ya muda mrefu na zile zinazohitilafiana na desturi za wakulima na wafugaji.

Ufumbuzi wa kuondoa migogoro ulilenga kwanza katika kuondoa tatizo la rushwa ili sheria zilizopo zitekelezwe kikamilifu. Mikakati iliyopendekezwa ni kuunda vikundi vya wakulima na wafugaji ili kujenga uwezo wa pamoja wa kutatua matatizo kisheria, elimu ya haki na sheria itolewe hadi vijijini, vijiji viwe na bajeti inayoonyesha matumizi halisi yanayotarajiwa ili viwe na uwezo wa kuwalipa watendaji wa vijiji. Aidha yaundwe mabaraza ya kijamii ya kutatua migogoro na kukemea wanaotoa au kupokea rushwa katika jamii bila kulazimika kwenda katika vyombo vya sheria.

Ufumbuzi mwingine ulilenga katika kuthibiti matumizi ya ardhi na maji. Ilipendekezwa kuwepo na mipango ya kitaifa ya matumizi bora ya ardhi. Kila kipande cha ardhi nchini kieleweke matumizi yake. Maeneo ya akiba kwa ajili ya upanuzi wa kilimo, ufugaji au shughuli nyingine yaeleweke na utaratibu wa kuyatumia pindi yanapohitajika ueleweke.

Tamko la warsha lilisisitiza kuwa taarifa za kazi za warsha iwafikie watendaji wakuu wa wizara za Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Mifugo, na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, serikali ichukue hatua za haraka na sahihi badala ya kungoja mapigano kutokea. Serikali ilishauriwa kufanya jitihada za makusudi kusambaza vijitabu vya sheria ya ardhi kwa wananchi na kuwahamasisha kuielewa.



*Baadhi ya washiriki wa warsha wakiwa kwenye zoezi la kutambua viini vya matatizo*

# 1. UTANGULIZI

## *1.1 Maandalizi ya warsha*

Warsha juu ya mahusiano baina ya wakulima na wafugaji wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliandaliwa na mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo (TARP II SUA) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Warsha ilifanyika katika kituo cha vijana wakatoliki Don Bosco mjini Songea. Washiriki wa warsha hiyo walikuwa wafugaji 8, wakulima 10 kutoka wilaya za Chunya, Mpanda, Mbeya vijijini, Mbarali, Njombe na Iringa vijijini. Kati yao wanawake walikuwa 5 na wanaume 13. Washiriki wengine walikuwa watafiti 3 kutoka kituo cha Utafiti cha Uyole Mbeya, na mwingine 1 kutoka SUA. Wengine walioshiriki ni Afisa Kilimo na Mifugo, Afisa Ardhi, Afisa Mipango wa Wilaya ya Mbarali, na mtendaji wa kata mmoja kutoka wilaya ya Mbarali. Aidha wataalamu wa ugani 5 kutoka maeneo yote waliyotoka wakulima na wafugaji walishiriki. Warsha pia ilijumuisha waandaaji wanne kutoka SUA na wawili kutoka kituo cha Utafiti Uyole Mbeya, na Mshiriki mmoja kutoka shirika lisilo la liserikali (NGO) la Intermon Oxfam ambaye ndiye alikuwa mwezeshaji wa warsha. Orodha na wasifu wa washiriki upo kwenye Kiambatanisho Na. 1.

Washiriki wa warsha hiyo walitoka kwenye maeneo yenye migogoro baina ya wafugaji na wakulima wa mazao katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Taarifa za mapigano baina ya wakulima wa mazao na wafugaji zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara kutokea katika maeneo hayo. Umwagaji damu, upotevu wa maisha ya watu na mali vimeripotiwa kutokea katika migogoro na mapigano hayo. Hali hii inaashiria ukosefu wa amani na utulivu katika jamii hizo. Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato Katika Kaya unaamini kuwa utulivu na amani ni nguzo muhimu katika kuifanya jamii kuwa na uhakika wa chakula na kipato. Hivyo, Mradi ulichukua jukumu la kuendesha warsha hii kama moja ya mikakati yake katika kutimiza malengo yake.

## *1.2 Madhumuni*

Lengo kuu la warsha hiyo lilikuwa ni kutafakari vyanzo vya machafuko baina ya wafugaji na wakulima katika wilaya za Mbarali, Mbeya vijijini, Chunya, Mpanda, Iringa vijijini na Njombe, na kubaini mbinu muafaka katika kuepuka migogoro hiyo. Hivyo, warsha ilikuwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kubainisha uhusiano yalivyo hivi sasa baina ya wakulima na wafugaji katika wilaya zilizowakilishwa kwenye warsha na kuainisha shida kuu iliyopo

ii. Kubainisha sababu za kuwepo kwa shida hiyo kuu, viini vyake na umuhimu wake katika kupewa kipaumbele

iii. Kupendekeza ufumbuzi, mikakati na wahusika katika utekelezaji wa mapendekezo yatakayotolewa.

## *1.3 Utambulisho na ufunguzi*

Washiriki waliwasili kwenye ukumbi wa warsha saa 2.30 asubuhi tarehe 26/11/2001. Washiriki walijitambulisha kwa majina, walikotokea na wasifu wao (Kiambatanisho Na. 1). Baada ya utambulisho washiriki walieleza matarajio yao kwa kuandika katika kadi. Matarajio ya washiriki yalikuwa ya aina kuu mbili kama ifuatavyo:

i. Kupata elimu juu ya kuboresha uzalishaji wa mazao na mifugo
   - Kufahamiana na kubadilishana uzoefu na washiriki wengine juu ya mbinu mbalimbali za uzalishaji wa mifugo na kilimo
   - Namna ya kuboresha ufugaji wa asili na utengaji bora wa maeneo ya malisho
   - Kuongeza ujuzi juu ya kilimo na ufugaji bora
   - Kuongeza maarifa juu ya kilimo na ufugaji wa kisasa
   - Kujua jinsi mkulima anavvoweza kuinua uchumi wake
   - Kupata elimu ambayo yawaelimisha waliowakilishwa
   - Kujua mtazamo wa wakulima na wafugaji juu ya utafiti wa kilimo na mifugo nchini
   - Kupata elimu itakayowezesha kuongeza ufanisi katika uzalishaji
   - Kufahamu juu ya matibabu ya mifugo
   - Kupata mawazo juu ya mipango bora ya matumizi ya ardhi
   - Kujua umuhimu wa mifugo ya asili katika swala la uhakika wa chakula na pato la kaya.

ii. Kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji
   - Kutambua viini vya migogoro baina ya wafugaji na wakulima
   - Kuelewa mbinu za kuepuka migogoro baina ya wafugaji na wakulima kutoka kwa waliowahi kuitatua
   - Kuwapatanisha wakulima na wafugaji
   - Kujua namnagani nitafanya iwapo mimi ni mkulima na ni mfugaji na wafugaji wanatakiwa kuhama eneo ninalokaa
   - Kupata uzoefu wa namna ya kutatua migogoro ya ardhi
   - Kujua mapendekezo ya namna ya kutatua migogoro yetu
   - Kuona namna gani wafugaji watakubali wasihamehame ovyo na kwa kutengewa eneo lao la kufugia
   - Kuona kama kuhamishwa kwa wafugaji kutaisha

Hatimaye Mgeni rasmi Afisa Kilimo na Mifugo, Bi. S.J.Msanga ambaye alimwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma katika ufunguzi wa warsha hiyo mara baada ya Mratibu wa Mradi Profesa L.D.B Kinabo alimkaribisha mgeni na kumtambulisha kwa washiriki. Mratibu wa mradi alimfahamisha mgeni rasmi pamoja na washiriki lengo na madhumuni ya Mradi. Baadaye alimkaribisha mgeni rasmi kuzungumza na washiriki.

Katika hotuba yake mgeni rasmi aliwasisitizia washiriki wa warsha kutumia fursa zinazotolewa na Mradi huo ili kuwawezesha watafiti wa SUA na wale wa Wizara ya Kilimo na uhakika wa chakula kufanya tafiti ambazo zitaleta matunda haraka iwezekanavyo. Mgeni rasmi aliifungua warsha rasmi na kupiga picha ya pamoja na washiriki.

# 2 KUAINISHA MATATIZO CHANZO NA KIPAUMBELE KATIKA UTATUZI

## *2.1 Kutathmini mahusiano baina ya wafugaji wa wakulima wa mazao*

Kila mshiriki alipewa fursa ya kuandika mahusiano mazuri na yale yaliyo mabaya anayoyaona kuwapo baina ya mkulima na mfugaji. Kila mshiriki alitakiwa kuonesha katika kadi zake kama yeye ni mkulima wa mazao, mfugaji, mtaalamu mwandamizi, mataalamu wa ugani au mtafiti na kufanya makusanyo ya maoni ya wanawarsha katika makundi hayo.

Maoni ya washiriki juu ya mahusiano mazuri na mabaya yaliyopo baina ya wafugaji na wakulima wa mazao yaliainishwa na kuwekwa katika makundi makubwa mawili. Yale yenye misingi ya kijamii na yale yenye misingi ya kiuchumi. Maoni yalikuwa kama ifuatavyo kwenye Jedwali.

| **HALI YA UHUSIANO ILIVYO BAINA YA WAKULIMA NA WAFUGAJI** | |
|---|---|
| **Kwa mtazamo wa wakulima** | **Kwa mtazamo wa wafugaji** |
| MAHUSIANO MABAYA KIJAMII | |
| 1. Kudharauliana | Mkulima kutokutaka maelewano mifugo inapoharibu mazao shambani |
| 2. Mifugo kuchafua vyanzo vya maji | Kutothamini mifugo |
| 3. Mfugaji ni jeuri | Kudharauliana |
| 4. Kuchukua sheria mkononi | Mfugaji kuonekana kama mvamizi |
| 5. Mfugaji kuuza mazao yenye magonjwa | Kutoshirikishwa katika uongozi na mipango ya matumizi ya ardhi na maji |
| 6. Mfugaji kutoa rushwa | Wakulima kuchukua sheria mkononi |
| 7. Wafugaji wanahamahama hivyo kutoshirikishwa katika mipango endelevu | Wakulima wana wivu |
| 8. Mfugaji kutothamini mazao | Wakulima kudai fidia kubwa kuliko kiasi cha uharibifu |
| 9. Mbinu mbaya za utatuzi wa migogoro kama vita au kutumia nguvu | Wakulima wanawategeshea wafugaji ili watoe (wafugaji) rushwa au fidia |
| 10. | Wakulima hawatupendi wamasai na hatujui kosa. |
| 11. | Chuki na kushinikizwa kuhama |

| | |
|---|---|
| 12. | Wafugaji wanabanwa kwenye maeneo madogo |
| 13. | Mbinu mbaya za utatuzi wa migogoro kama vita na nguvu |

| | |
|---|---|
| MAHUSIANO MAZURI KIJAMII | |
| 1. Mifugo kutumika katika mahari na sherehe mbalimbali | Mifugo kutumika katika mahari na sherehe mbalimbali |
| 2. Kusaidiana katika matatizo ya kijamii kama misiba na sherehe | Kusaidiana katika matatizo ya kijamii kama misiba na sherehe |
| 3. Kuoleana hasa wafugaji kuoa kwa wakulima | Kushirikiana katika kuelimisha watoto. Wakulima hukaa na watoto wa wafugaji wanaokwenda shule wakati wazazi wao wamehama kutafuta malisho |
| 4. | Mikutano ya pamoja |
| 5. | Kuoleana |
| MAHUSIANO MABAYA KIUCHUMI | |
| 1. Mifugo kuharibu mazao | Mkulima kulima eneo la machungo au njia ya kupitisha mifugo |
| 2. Kugombea ardhi na maji hasa maji | Kugombea ardhi na maji hasa maji |
| 3. Wafugaji wenye makundi makubwa huharibu mazingira | Kuweka sumu kwenye mazao ili wanyama wakila wafe |
| 4. Mifugo kuharibu mifereji ya maji | Kufinya (kupunguza) maeneo ya kuchungia |
| 5. Mifugo kuleta magugu shambani | Kukata miti na kutayarisha mashamba yasiyo ya kudumu |
| 6. Kushoma moto ili kuandaa malisho | Wakulima kulima kwenye vyanzo vya maji |
| 7. Kukata miti ya kutenegenezea maboma ya mifugo yasiyo ya kudumu na kufukuza ndorobo | Mkulima kuchoma moto bila uamgalifu wakati wa kutayarisha mashamba na hivyo kuunguza malisho. |
| MAHUSIANO MAZURI KIUCHUMI | |
| 1. Kupata mbolea | Kuazimana ng'ombe wa kulimia na kazi zingine |
| 2. Kupata maziwa na nyama | Kupata chakula |
| 3. Kununua mifugo kwa shughuli za kijamii | Kupata soko la maziwa na nyama |
| 4. Mifugo kutumika kama nguvu kazi | Kupata mbolea |

| | |
|---|---|
| katika shughuli za kilimo na usafirishaji | |
| 5. | Kutoa huduma ya kulimia mashamba |
| 6. | Kushirikiana kusaka wezi wa mifugo |
| 7. | Kumkopesha mkulima |
| 8. | Kupata mabua ya kulishia mifugo |
| 9. | Kumwazima mkulima ng'ombe wa kukamua maziwa. |

Baada ya kutafakari mahusiano yalivyo, wanawarsha walibaini kuwa japokuwa yapo mahusiano mazuri mengi baina ya wakulima na wafugaji, kiwango cha madhara na mashaka ya maisha kinachosababishwa na mahusiano mabaya kinafanya mahusiano kwa ujumla kuwa MABAYA. Hivyo tatizo kuu ambalo wanawarsha walilibaini kuwepo baina ya wakulima na wafugaji ni mahusiano mabaya baina yao.

## *2.2 Maelezo kuhusu mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo*

Baada ya shida kuu kujulikana washiriki walijifunza kwa ufupi kuhusu mbinu ya ufumbuzi yakinifu wa matatizo. Mbinu ambayo wataituma katika kutafuta sababu za kuwepo kwa tatizo kuu lililobainishwa, viini vyake na umuhimu wake. Mada hiyo ilifundishwa kwa kutumia kielelezo cha mfano hai wa shida ya **ajali nyingi za barabarani** (Kiambatisho Na. 2). Baada ya washiriki kuonesha kuwa wameielewa mbinu hiyo waliendelea na hatua zilizofuata.

## *2.3 Kubainisha matatizo, jinsi yanavyohusiana na umuhimu wake katika kipaumbele*

Washiriki walikubaliana kuunda vikundi sita ili kufanikisha zoezi la kubaini matatizo chanzo ya **mahusiano mabaya** baina ya wakulima na wafugaji, kutambua yanavyohusiana na viini vyake. Makundi hayo yalikuwa yafuatayo:

1. Kikundi cha wakulima wa wilaya za mkoa wa Mbeya
2. Kikundi cha wakulima wa wilaya za mikoa ya Iringa na Rukwa
3. Kukundi cha wafugaji wa wilaya za mkoa wa Mbeya
4. Kikundi cha wafugaji wa wilaya za mikoa ya Iringa na Rukwa
5. Kikundi cha wataalamu, watafiti na wataalamu wa ugani ( kilimo na mifugo)
6. Kikundi cha wataalamu waandamizi wa wilaya ya Mbarali

Majadiliano ya vikundi yaliwezesha kila kikundi kuorodhesha matatizo yanayosababisha kuwepo kwa tatizo kuu la mahusiano mabaya baina ya wafugaji na wakulima. Kila kikundi kilipata fursa ya kuwasilisha orodha ya matatizo waliyobainisha kwa

wanawarsha wote. Wanakikundi walifafanua mazingira ya kila tatizo waliloorodhesha kadri ya uwezo wao na kuwaelewesha wanawarsha wengine.

Baadaye wanawarsha walirejea katika vikundi vyao na kutumia mbinu ya **utatuzi yakinifu** waliyojifunza kuyapanga matatizo waliyoainisha katika mchoro unaoonesha jinsi matatizo hayo yanavyohusiana katika kusababishana. Hatimaye waliweza kubainisha matatizo **viini** na kuyapatia kipaumbele. Kila kikundi kiliweza kutengeneza mchoro wa uchambuzi yakinifu kama inavyoonekana kwenye Viambatanisho Na. 3a-f.

Kwa ujumla matatizo chanzo na viini vya tatizo kuu yalikuwa yanafanana katika makundi yote japokuwa kila kundi lilikuwa na mtazamo wake kuhusu matatizo hayo. Matatizo hayo yamegawanyika katika tabaka tatu zinayohusu:

i. Matumizi ya rasilimali hasa ardhi na maji
ii. Utendaji wa viongozi na serikali
iii. Tofauti za kijamii

Matatizo hayo yanaripotiwa pamoja na mitazamo ya kila kundi lililowakilishwa kwenye warsha.

### 2.3.1 Matumizi ya rasilimali hasa ardhi na maji

*i. Mwingiliano katika matumizi ya ardhi*

Hali ya mkulima au mfugaji kuingia katika eneo la mwingine ama kwa makusudi au bila kujua na kusabisha uharibifu. Mara nyingi mwingiliano huo husababisha uharibifu wa mazao. Wafugaji pia wamepoteza mifugo yao kutokana na kula mimea yenye sumu au mifugo kuumizwa na wakulima kama vile kukatwa mikia.

*ii. Mifugo kuharibu mazao*

Vikundi vyote vilikuwa na mtazamo wa aina moja kuhusu tatizo hilo. Matukio ya mifugo kuingia kwenye mashamba yenye mazao hutokea mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa mazao.

*iii. Ng'ombe wengi kuliko malisho*

Tatizo hilo pia lilitazamwa kwa mtazamo sawa kwa makundi yote kuwa ng'ombe wanafugwa na kuchungwa kwenye maeneo ambayo hayatoshelezi mahitaji yao na hivyo kufanya **malisho na maji kuwa haba.**

*iv. Wakulima kujiona wenye ardhi*

Wafugaji wanaona kuwa hali iliyopo ya wakulima kuamua kufungua mashamba mahali popote hata kama eneo hilo hutumiwa kwa ajili ya malisho ya mifugo ni kielelezo kinachoonesha kuwa wakulima wanajiona kuwa na haki juu ya kutumia ardhi kuliko wafugaji. Wafugaji wanaona kuwa hali hiyo ni **uvamizi wa wakulima kulima maeneo ya malisho.** Hata serikali za vijiji huchukulia kuwa maeneo ya malisho ya mifugo ni hifadhi ya ardhi kwa upanuzi wa kilimo. Hivyo inapohitajika kugawa maeno mapya kwa wakulima maeneo ya upanuzi huo huwa pamoja na yale yaliyopangwa kwa ajili ya malisho ya mifugo. Matokeo yake maeneo ya kufugia mifugo huzidi kubanwa.

v. *Maeneo mazuri kwa kilimo na malisho kuwa madogo*

Washiriki wote walibaini kuwa maeneo mazuri yanayofaa kwa kilimo ndiyo pia yanayofaa kwa malisho. Na kwa bahati mbaya sehemu za aina hiyo ni chache ukilinganisha na mahitaji. Matokeo yake huwa ni msongamano wa mifugo na mashamba katika sehemu za aina hiyo. Wataalamu waliliona tatizo hilo kwa mtazamo wa kutokuwa na utaalamu wa kutosha katika ufugaji na kilimo miongoni mwa wakulima na wafugaji, hivyo kutegemea zaidi ubora wa asili wa raslimali. Hata hivyo, walikiri kuwa takwimu sahihi za uwezo wa nchi katika ufugaji na kilimo hazipo. Kwa mfano inaonekana kuwa **ongezeko la watu na mifugo** limekuwa tatizo lakini haijulikani kama uwezo wa nchi unamudu ongezeko zaidi au la.

vi. *Kugombania ardhi*

Wakulima na wafugaji wamejikuta wakigombea maeneo huku kila mmoja akijiona ana haki juu ya eneo husika. Hali hii hujitokeza zaidi kwenye maeneo ambayo awali hayakuwa ya kilimo wala ufugaji.

vii. *Kuchoma moto ovyo*

Washiriki wote walikubaliana kuwa uchomaji moto wa misitu na nyika unachangia kupunguza maeneo ya malisho. Wafugaji wanaona wakulima kuwa wachomaji zaidi wa moto hasa wakati wanapotayarisha mashamba na wengine hufanya makusudi ili kuharibu malisho kwa ajili ya kuwafukuza wafugaji. Hivyo malisho yanapokuwa yameungua mfugaji hulazimika kutafuta malisho mahali popote na hivyo kujikuta wanaingia kwenye maeneo ya kilimo.

Wakulima kwa upande wao wanaona wafugaji kuwa ndio wachomaji zaidi wa moto kwa kile wanachodai kuwa kutayarisha malisho mapya. Pia kufukuza ndorobo. Kabla malisho mapya hayajapatikana wafugaji hulazimika kuingiza mifugo kwenye maeneo ya mashamba na hivyo kuzusha migogoro.

viii. *Kilimo na ufugaji wa kuhamahama*

Uhamishaji wa mifugo kutoka eneo moja hadi jingine kutafuta malisho ni tatizo ambalo kila mshiriki alikiri kuwa lipo. Mifugo imedaiwa kuhamishwa bila utaratibu na hivyo kujikuta mifugo mingi inachungwa kwenye eneo dogo na ambalo pia linatumiwa kwa kilimo. Makundi makubwa ya ng'ombe yanapohama huharibu mazao na maliasili njiani wanakopita. Hata hivyo wafugaji walidai kuwa hulazimika kuhama kutokana na mabadiliko ya hali ya mazingira kwa kila msimu. Kwa mfano, wakati wa masika mifugo hupata malisho ya kutosha sehemu za milimani (miinuko) ambako kwa kawaida mashamba pia ni machache au hakuna kabisa. Wakati huo sehemu za mabonde hazifai kabisa kwa kuchungia sababu ya tope jingi. Wakati huo wakulima hulima mazao hasa mpunga kwenye maeneo hayo ijapo yametengwa kwa ufugaji.

Kiangazi kinaporejea malisho sehemu za milimani (miinuko) huisha sababu ya ukame. Malisho mazuri huwa mabondeni na hivyo hulazimika kurudi mabondeni kupata malisho mazuri na maji. Tatizo huzuka pale mifugo inapowahi kurudi kabla mazao hayajavunwa, au wakulima kuwahi kulima kabla mifugo haijahama

yote, au mkulima kuamua kulima mazao ya kiangazi kwenye mabonde ambayo wachungaji huyategemea kwa malisho wakati wa kiangazi.

Pia ilionekana kuwa wakulima huhamahama kutafuta rutuba nzuri. Wakati mwingine wakulima huhamia kwenye maeneo ya malisho kwa kuwa huko kuna urutubisho wa samadi ya wanyama. Huko hulazimika kupambana na wafugaji ambao huona kuwa wameingiliwa.

Wataalamu kwa upande wao waliona kuwa kuwapo kwa maeneo huria ambayo yanajulikana kama maeneo ya umma hufanya wakulima na wafugaji wajione huru kuhama wakati wowote na mahali popote ilimradi ni ardhi ya umma. Hata haja ya kutumia utaalamu hukosekana. Hivyo kujikuta wanagombea ardhi ambayo kila mmoja anajiona kuwa ana haki nayo zaidi ya mwenziwe.

ix. *Ufugaji/kilimo visivyo vya utaalamu*

Washiriki wote walikiri kuwa mbinu zinazotumiwa na wakulima na wafugaji ni duni. Wakulima hawajali kilimo cha kuhifadhi rutuba na hivyo kulazimika kupanua maeneo ili kufidia upungufu wa mavuno unaotokana na upungufu wa rutuba ya ardhi. Hivyo kujikuta wameingia katika maeneo ya wafugaji na kusababisha migogoro.

Wafugaji pia wanathamini ongezeko la mifugo bila kujali hifadhi ya malisho. Mifugo inapoongezeka hulazimika kuhama kutafuta malisho zaidi na hivyo kusababisha migogoro. Hata hivyo wafugaji wanakiri kuwa iwapo ufugaji wa kitaalamu maana yake ni kufuga mifugo michache basi hilo pia ni tatizo jingine kwao. Wingi wa mifugo kwao ni uhakika wa maisha. Hata hivyo, wataalamu kwa upande wao pamoja na kukiri kuwa ufugaji wa kitaalamu unakuwa mgumu mifugo inapokuwa mingi, upo uwezekano wa mfugaji kufuga mifugo mingi kitaalamu kama vile ranchi za taifa wanavyofanya.

x. *Wachungaji kutokuwa makini*

Wakulima walibaini kuwa baadhi ya wachungaji si waangalifu. Huachia mifugo yao kuingia kwenye mashamba ya wakulima kwa uzembe.

xi. *Wachungaji jeuri*

Washiriki walikiri kuwa wapo wachungaji ambao ni jeuri. Hulazimisha kuingiza mifugo yao kwenye mashamba yenye mazao kwa nguvu. Wakati mwingine hutishia wenye mashamba kwa silaha kama sime na mikuki. Mwenye shamba anapozuia mifugo hiyo mapambano hutokea na hata kusababisha umwagaji wa damu. Hata hivyo, ilibainika kuwa jeuri hiyo kwa kiasi kikubwa husababishwa na baadhi ya wenye mifugo ambao huwahamasisha wachungaji wao kushibisha mifugo yao hata kama ikibidi kwenye mashamba yenye mazao na kuwaahidi kuwa wapo tayari kulipa au kusimamia kesi mahali popote iwapo watashitakiwa.

### 2.3.2 Utendaji wa viongozi na serikali

*i. Serikali kugeuza maeneo kuwa hifadhi au kufungua miradi kwenye maeneo ya wakulima au malisho*

Wakulima na wafugaji wanaona kuwa utaratibu wa serikali wa kuamua kutenga maeneo kuwa hifadhi bila kujali waliokuwa wakiyatumia maeneo hayo watakwenda wapi ni tatizo linalosababisha uhaba wa maeneo ya kilimo. Mfano ni utengaji wa hifadhi ya Ruaha. Wakati mwingine serikali imeanzisha miradi inyohodhi ardhi kubwa bila kujali maslahi ya wakulima na wafugaji waliokuwa wanatumia maeneo hayo. Hali hiyo huwalazimisha wakulima na wafugaji waathirika kuvamia maeneo mengine na hivyo kusababisha migogoro.

*ii. Utaratibu mbaya wa kugawa ardhi*

Wafugaji wanaona kuwa uwiano wa ardhi wanayogawiwa kwa kuchungia si sawa na mahitaji yao. Mahali pengine vijiji vimetengwa vya wafugaji na vingine vya wakulima bila kujali masilahi ya wakulima ambao ni wafugaji. Mkulima mwenye mashamba katika eneo ambalo limegawiwa kuwa la ufugaji pia haijulikani aende wapi. Matokeo yake mkulima mwenye mashamba katika kijiji kilichotengwa kwa kufugia hulazimika kuendelea kulima kijijini hapo na hasa anapoona kuwa wafugaji wenyewe ndani ya kijiji cha wafugaji nao wanalima mashamba haoni kwa nini yeye (mkulima) aondoke.

Hata serikali kuu haina utaratibu unaoonesha kuwa mifugo ikizidi eneo moja iende wapi. Au wakulima wakizidi eneo moja wahamie wapi. Hii inatokana na serikali kutokuwa na mipango ya kitaifa ya matumizi ya ardhi. Kama ipo iko kwenye mafaili tu na walengwa hawaijui au haikidhi haja halisi iliyopo. Tatizo hilo huchangia katika migongano ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji. Wakulima na wafugaji wamejikuta wakigombea maeneo ambayo awali hayakuwa chini ya kijiji chochote na serikali haijatamka kama maeneo hayo ni kwa matumizi gani. Wala utaratibu wa kuyatumia maeneo hayo haueleweki. Inapotokea serikali imepata mradi wa kufanya katika maeneo ya aina hiyo huwafukuza wananchi wanaokuwemo na kusababisha mgongano zaidi katika maeneo mengine ambako wananchi hao hulazimika kuhamia.

*iii. Suluhu kukosekana*

Warsha ilibaini kuwa mara nyingi migogoro hutokea pale suluhu inapokosekana baina ya mkulima na mfugaji mifugo inapoharibu shamba la mkulima. Hali hiyo hutokea pale ambapo mfugaji anapoona kuwa hana hatia au hatia aliyonayo ni ndogo kuliko fidia anayotakiwa kutoa. Baadhi ya wafugaji wakorofi hawahitaji suluhu na kutamba kuwa mkulima ni mnyonge hawezi kufanya chochote hata haki yake hawezi kuipata akiidai kisheria.

*iv. Utekelezaji mbaya wa mipango ya serikali*

Warsha ilibaini kuwa wakati mwingine serikali ina mipango mizuri,lakini utekelezaji wake unakuwa mbaya. Mfano ni sera ya wanyama pori na hifadhi za taifa inayosisitiza ushirikishwaji wa wakazi wa maeneo husika yanayohitaji kutengwa kwa ajili ya hifadhi ya taifa. Warsha iliridhika kuwa utekelezaji wa sera

hiyo katika zoezi la utengaji wahifadhi ya taifa ya Ruaha haukuzingatia sera ilivyotamka.

Hata hivyo mipango mingine ya serikali ni migumu kuitekeleza kwa vile inahitaji rasilimali ambazo huwa vigumu kupatikana. Mpango wa matumizi ya ardhi ni mfano mmoja wapo. Mpango huo unatekelezwa kikamilifu mijini kuliko vijijini. Vijiji vingi havina uwezo wa kumudu gharama za upimaji wa ardhi. Njia za asili za kutenga mipaka haziwezi kukidhi haja ya kukiwezesha kijiji kutathmini kiwango cha ubora na ukubwa wa ardhi na maji ambavyo vipo kijijini. Kwa kutumia njia za upimaji za asili, kijiji hakiwezi kujua uwezo halisi wa kijiji kumudu ufugaji na kilimo cha mazao. Hivyo utengaji wa maeneo ya ufugaji na kilimo wa asili umeshindwa kukidhi haja iliyopo ya vijiji kupanga mipango sahihi ya matumizi ya ardhi yake.

Halmashauri za wilaya ambazo zimepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa zoezi la mipango ya matumizi ya ardhi vijijini pia hazina uwezo wa kutekeleza mpango huo kutokana na mapato yao kuwa madogo.

v. *Vyombo vya haki vya kata kutojua sheria*

Warsha ilibaini kuwa uelewa wa sheria katika vyombo vya dola ngazi ya kata ni mdogo. Hii imefanya migogoro mingi kushindwa kutatuliwa kwa vile waathirika hushindwa kuridhika na maamuzi yanayotolewa kwenye ngazi ya kata.

vi. *Rushwa*

Warsha iliridhika kuwa yapo mazingira yanayoonesha kuwepo kwa rushwa inapotokea migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Watafiti na viongozi waandamizi walikuwa na mtazamo kuwa haraka ya wahusika katika migogoro ya kumaliza mambo yao inafanya mazingira ya rushwa kuwepo.

Wakulima kwa upande wao waliona kuwa jeuri ya mali waliyonayo baadhi ya wafugaji ni dalili ya kuwepo kwa rushwa. Wakulima walitaja mifano kama vile wachungaji kuingiza mifugo kwa nguvu shambani na kumuamuru mkulima aende popote kushitaki kwa vile wao (wachungaji) wanauhakika hawatachukuliwa hatua zozote. Na kweli hatimaye hawafanywi chochote japokuwa mkulima muathirika hupeleka malalamiko yake katika vyombo vya sheria.


Wafugaji nao walikubaliana na kuwepo mazingira ya rushwa. Wafugaji walibainisha kuwa vyombo vya dola vinavyosimamia sheria na utoaji wa haki hasa polisi na mahakama vimewageuza wafugaji kuwa **'vimbotela'**. Kimbotela ni neno la Kimbugu lenye maana ya shimo la dhahabu lenye utajiri mkubwa ambalo kila mchimbaji hakosi kujipatia chochote kwa muda mrefu. Hivyo wafugaji wanajiona kugeuzwa vimbotela na watendaji wasimamizi wa haki na sheria. Washiriki wa warsha kutoka Chunya walitoa kielelezo kifuatacho kuonesha jinsi mzunguko wa rushwa ulivyo na unavyofananishwa na Kimbotela.

Kielelezo hiki kinaonesha kuwa uharibifu unapotokea mlalamikaji huenda kutafuta haki yake kwenye vyombo vya dola. Kule kwenye ngazi ya kata

hulazimika kutoa fedha ili kikao kiweze kufanyika kwa kuambiwa kuwa 'asafishe kiwanja cha mkutano'. Mlalamikiwa anapofuatwa, hukamatwa na kutishiwa na pia kuwekewa ukiritimba unaomlazimu kutoa fedha kwa wahusika. Vitisho vinavyo tolewa ni kama vile 'hatuna usafiri wa kwenda kushuhudia tukio, ama utawekwa rumande muda usiojulikana mpaka upelelezi utakapokwisha, ama kesi yako ni mbaya utafungwa miaka kadhaa au kutozwa faini kubwa sana. Mtuhumiwa akishatoa fedha kiasi cha kuridhisha huambiwa hana kesi arudi nyumbani.

Mlalamikaji akifuatilia kesi yake hujitokeza mtendaji mwingine kwenda kumkamata upya mtuhumiwa. Ukiritimba na vitisho huanza tena mpaka hapo mtuhumiwa atakapotoa fedha za kuzimisha moto. Hali hiyo huendelea mpaka hapo mlalamikaji atakapokata tamaa. Hali hii husababisha chuki baina ya mlalamikaji na mlalamikiwa. Mlalamikaji humwona mlalamikiwa kama mgandamizaji kutokana na uwezo wake wa kutoa fedha. Mtuhumiwa humwona mlalamikaji kama mchochezi anayemsababishia kupoteza fedha na mali nyingi bila sababu.

**Kielelezo cha mzunguko wa rushwa unaofananishwa na "kimbotela" yaani shimo la dhahabu**




Hali hiyo imefanya baadhi ya jumuiya za wafugaji kuanzisha mifuko ya fedha ya kusaidiana kumaliza matatizo yao ama kwa kukidhi haja ya usafishaji viwanja ama

kulipa faini na fidia pale inapolazimu. Kipindi hicho huwa ni kile ambacho malisho na maji ni haba na kwamba uwezekano wa mifugo kuingia katika maeneo yasiyostahili ni mkubwa. Wakulima wanaiona hali hiyo ya ushirikiano wa wafugaji kujenga uwezo wa kifedha ni mwanya wa rushwa na unaozidisha jeuri ya fedha miongoni mwa jamii za wafugaji.

Kukithiri kwa rushwa namna hiyo kumepelekea matatizo mengi kugeuka kuwa migogoro mikubwa kutokana na vyombo vya dola kutotatua matatizo hayo kikamilifu. Mara nyingi vyombo hivyo hutoa maamuzi yanayoonekana kuwa si ya haki na hivyo kupelekea upande mmoja kutoridhika. Tatizo la aina hiyo likijitokeza tena upande ambao haukuridhishwa na maamuzi ya awali, huamua kuchukua sheria mkononi kama vile kuumiza mifugo, wachungaji na wakulima mashambani hasa watoto na kinamama.

### 2.3.3 Mahusiano ya kijamii

*i. Tamaa ya wakulima kutaka kulipwa*

Wafugaji walibaini kuwa baadhi ya wakulima huwa na tamaa ya kutaka kulipwa. Hufungua mashamba kwenye maeneo ambayo wanahakika mifugo hupita ili wapate fidia kubwa iwapo mazao yao yataharibiwa. Wengine hudiriki kulazimisha mifugo kuingia mashamabani mwao ili wadai fidia ya uharibifu.

*ii. Wakulima na wafugaji kutojua sheria*

Uelewa mdogo wa sheria na haki baina ya wakulima na wafugaji hupelekea waathirika katika migogoro kudhani kuwa wameonewa au kushindwa kufuatilia haki zao. Hali hii husababisha chuki baina ya waathirika wao kwa wao na pia baina yao na vyombo vya sheria na haki. Washiriki wa warsha walikubaliana wote juu ya jambo hilo.

*iii. Wachungaji jeuri*

Baadhi ya wachungaji ni jeuri. Wakulima walibaini kuwa wachungaji wengine huingiza mifugo kwenye mashamba na kuharibu mazao kwa nguvu. Wachungaji wa aina hiyo hudai kuwa thamani ya mifugo wanayoaangalia ni kubwa sana kulinganisha na mazao yanayoharibiwa hivyo mkulima hapaswi kulalamika na kwamba ana hiari ya kufanya atakavyo. Wafugaji walikubaliana kuwepo kwa hali hiyo. Lakini waliona kuwa hiyo ni tabia ya baadhi ya wachungaji wanaozuzuliwa na idadi ya mifugo wanayochunga wakidhani kuwa kuuzwa ngo'mbe mmoja au wawili kati ya mamia ya ngombe wanaowachunga si kitu. Wafugaji hawakukubaliana na hoja kuwa wenye mifugo huendekeza jeuri hiyo ya wachungaji wao. Walibaini kuwa wafugaji huumia sana wanapolazimika kupoteza ng'ombe hata mmoja kulipa fidia kutokana na uzembe wa wachungaji. Hata hivyo walikiri kuwa wapo wafugaji wachache wenye jeuri kama wachungaji wao ambao huendekeza kiburi kwa wachungaji wao.

Ilionekana pia kuwa wachungaji wengine si makini katika kuangalia mifugo yao. Wachungaji wenye umri mdogo chini ya miaka 18 ndio wenye tatizo hilo.

iv. *Mila na desturi potofu*

Desturi ya wafugaji kupenda sifa ilionekana kuwa ni kichocheo cha wafugaji kufuga mifugo wengi kuzidi uwezo. Hiyo pia huchangiwa na mila na desturi zilizopitwa na wakati. Ilionekana kuwa kasumba ya kutaka kuwa na ngombe wengi kuzidi uwezo huwafanya wafugaji wengine kuwa watumwa wa mifugo bila wao kujitambua huku wakisababisha migogoro. Wafugaji wa aina hiyo hudhani wanafuga kumbe wana chunga (watumishi wa mifugo).

Mila za kuhamahama pia zimepitwa na wakati. Mila hizo ni jadi ya wafugaji. Ilibainika kuwa hata wakulima pia wanazo desturi za kuhama hama katika ulimaji.

Mila za wafugaji kutembea na silaha na kujiona kuwa wao ni wenye nguvu (katika mapigano na kiuchumi) ilionekana pia husababisha wafugaji wakorofi kunyanyasa wakulima wanyonge.

v. *Elimu duni ya wakulima na wafugaji*

Elimu duni iliwekwa katika tabaka kuu mbili.

- Hali ya kutojua kusoma na kuandika inayopelekea wakulima na wafugaji kushindwa kufuatilia maelekezo ya kilimo na ufugaji wa kitaalamu. Pia kutoona haja ya kubadilisha mfumo wa maisha na uzalishaji.
- Hali ya kutotumia utaalamu katika uzalishaji hata kama mkulima na mfugaji anajua kusoma na kuandika. Hali hiyo ilionekana kuchangiwa na
  - kuwepo kwa teknolojia zisizotekelezeka kwa urahisi, zinazohitaji gharama kubwa na mafunzo ya muda mrefu, na zile zinazohitilafiana na desturi za wakulima na wafugaji. Kwa mfano technolojia nyingi zinasisitiza matumizi ya pembejeo za viwandani ambazo ni ghali, si za uhakika, na zina viwango hafifu vya ubora. Mara nyingi wataalamu hushauri wafugaji wapunguze mifugo na kuwa ufugaji bora ni ule wa kuchungia ndani. Utaalamu wa aina hiyo hauchukuliki na mfugaji wa asili ambaye mifugo ni benki na dhamana ya kijamii.
  - Kuwepo fursa ya upanuzi holela wa maeneo ya uzalishaji. Mfano kama mfugaji au mkulima anaona lipo pori au mbuga isiyo na 'mwenyewe' mahali fulani, haitazamiwi mkulima huyo au mfugaji kuona haja ya kutumia kwa ufanisi na kwa uendelevu ardhi anayoitumia.

vi. *Ushiriki mdogo wa jamii za wafugaji katika serikali*

Ilionekana kuwa wafugaji wengi hawapendi kushiriki katika uongozi wa serikali hasa za vijiji. Hali ambayo hupelekea masilahi yao kutozingatiwa katika mipango na maamuzi ya serikali za vijiji.

xii. *Mfumo mbaya wa umilikaji ardhi*

Baadhi ya wananchi hasa wakulima ambao wao huona kuwa ndio wenye asili ya umilikaji wa mashamba, huhodhi mapori au mbuga kubwa kuliko uwezo wao na kudai kuwa walirithi kutoka kwa mababu zao.

## *2.4 Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi*

Kila kundi lililowakilishwa kwenye warsha lilibaini viini vya matatizo yanayosababisha mahusiano baina ya wakulima na wafugaji kuwa mabaya kwa kutumia mbinu ya upembuzi yakinifu. Michoro kwenye Viambatanisho Na. 3 a – f inaonesha kila kikundi kilichowakilishwa jinsi wanavyoona uhusiano wa matatizo yaliyobainishwa, viini vyake na kipaumbele kwa utatuzi wa kila kiini. Matatizo yaliyozungushiwa miduara miwili (ambayo hayana mishale inayoelekea kwayo) ndiyo matatizo viini. Kila kikundi kilitumia kete mia kuzigawanya katika michoro kama inavyoonekana kwenye Viambatanisho 3a – d. Wingi wa idadi ya kete zilizowekwa kwenye kila mduara wa tatizo umeoneshwa kwa namba zilizoko ndani ya miduara. Wingi wa kete unaashiria umuhimu au uzito wa tatizo. Tatizo kiini lenye idadi kubwa ya kete ndilo linaloonekana kuwa linalohitaji utatuzi wa haraka. Kila kundi lililowakilishwa lilionesha uhusiano na kipaumbele cha utatuzi kama ifuatavyo:

### 2.4.1 **Kikundi cha wafugaji kutoka wilaya za Mbeya**

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 1: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wafugaji kutoka wilaya za Mbeya**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 40 |
| 2. | Utaratibu mbaya wa ugawaji wa ardhi | 40 |
| 3. | Serikali kugeuza maeneo kuwa hifadhi au kufungua miradi | 18 |
| 4. | Tamaa ya wakulima kutaka kulipwa | 2 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi.*

Matarajio ya wafugaji wa wilaya za Mbeya ni kuwa iwapo rushwa itaondolewa:

- Vyombo vya sheria vitatekeleza wajibu wao
- Hivyo suluhu kupatikana wakati wote
- Na mahusiano kuwa bora

Iiwapo kutakuwa na utaratibu mzuri wa ugawaji wa ardhi:

- Maeneo mazuri kwa kilimo na ufugaji yatatumiwa vizuri
- Uvamizi wa wakulima katika maeneo ya malisho utakoma
- Wafugaji watafuga kwa uwiano sahihi na meneo yaliyopo
- Malisho yatakuwa ya kutosha na
- Hivyo mwingiliano katika matumizi ya ardhi hautakuwepo na uharibufu wa mazao na mifugo hautatokea.

## *2.4 Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi*

Kila kundi lililowakilishwa kwenye warsha lilibaini viini vya matatizo yanayosababisha mahusiano baina ya wakulima na wafugaji kuwa mabaya kwa kutumia mbinu ya upembuzi yakinifu. Michoro kwenye Viambatanisho Na. 3 a – f inaonesha kila kikundi kilichowakilishwa jinsi wanavyoona uhusiano wa matatizo yaliyobainishwa, viini vyake na kipaumbele kwa utatuzi wa kila kiini. Matatizo yaliyozungushiwa miduara miwili (ambayo hayana mishale inayoelekea kwayo) ndiyo matatizo viini. Kila kikundi kilitumia kete mia kuzigawanya katika michoro kama inavyoonekana kwenye Viambatanisho 3a – d. Wingi wa idadi ya kete zilizowekwa kwenye kila mduara wa tatizo umeoneshwa kwa namba zilizoko ndani ya miduara. Wingi wa kete unaashiria umuhimu au uzito wa tatizo. Tatizo kiini lenye idadi kubwa ya kete ndilo linaloonekana kuwa linalohitaji utatuzi wa haraka. Kila kundi lililowakilishwa lilionesha uhusiano na kipaumbele cha utatuzi kama ifuatavyo:

### 2.4.1 **Kikundi cha wafugaji kutoka wilaya za Mbeya**

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 1: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wafugaji kutoka wilaya za Mbeya**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 40 |
| 2. | Utaratibu mbaya wa ugawaji wa ardhi | 40 |
| 3. | Serikali kugeuza maeneo kuwa hifadhi au kufungua miradi | 18 |
| 4. | Tamaa ya wakulima kutaka kulipwa | 2 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi.*

Matarajio ya wafugaji wa wilaya za Mbeya ni kuwa iwapo rushwa itaondolewa:

- Vyombo vya sheria vitatekeleza wajibu wao
- Hivyo suluhu kupatikana wakati wote
- Na mahusiano kuwa bora

Iiwapo kutakuwa na utaratibu mzuri wa ugawaji wa ardhi:

- Maeneo mazuri kwa kilimo na ufugaji yatatumiwa vizuri
- Uvamizi wa wakulima katika maeneo ya malisho utakoma
- Wafugaji watafuga kwa uwiano sahihi na meneo yaliyopo
- Malisho yatakuwa ya kutosha na
- Hivyo mwingiliano katika matumizi ya ardhi hautakuwepo na uharibufu wa mazao na mifugo hautatokea.

Ugawaji mzuri wa ardhi pia:

- Utakomesha tabia ya baadhi ya wakulima kujiona wenye ardhi
- Na hivyo kuwafanya wasiwe na madai kwa ardhi ambayo si yao.

### 2.4.2 Wafugaji

i. *Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Jedwali Na 2. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa wafugaji wa kutoka wilaya ya Bagamoyo.

**Jedwali Na. 2: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wafugaji wa Mikoa ya Iringa na Rukwa**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 52 |
| 2. | Uchomaji moto ovyo | 20 |
| 3. | Ufugaji/kilimo visivyo vya kitaalamu | 18 |
| 4. | Ongezeko la watu | 10 |

i. *Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wafugaji wa mkoa ya Iringa na Rukwa wanaona kuwa iwapo rushwa itakwisha:

- Migogoro itapata suluhu
- Na hivyo kuimarisha mahusiano

Iwapo uchomaji moto holela hautakuwepo:

- Uharibifu wa malisho utakoma
- Na hivyo kupunguza ugombeaji wa ardhi na kuepuka mifugo kuharibu mazao
- Hivyo migogoro inyohitaji usuluhishi itapungua

Iwapo wakulima na wafugaji watazalisha kwa utaalamu:

- Wafugaji watafuga kwa uwiano wa maeneo
- Uhaba wa malisho utapunguza tatizo la kilimo na ufugaji wa kuhamahama
- Ugomvi wa ardhi na mifugo kuharibu mazao utapungua
- Migogoro inayohitaji usuluhisho itaepukwa.

### 2.4.3 Wakulima wa Mpanda na Njombe

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 3: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wa Mpanda na Njombe**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 70 |
| 2. | Elimu duni na kutotumia utaalamu katika uzalishaji | 60 |
| 3. | Wananchi kutoshirikishwa katika mipango ya maendeleo | 60 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wakulima wa Mpanda na Njombe waliona kuwa iwapo rushwa itakomeshwa:

- Kutakuwepo maelewano ya dhati kila uharibifu au mgogoro unapotokea.

Iwapo wakulima na wafugaji watatumia utaalamu katika uzalishaji:

- Wafugaji watafuga kwa uwiano na maeneo
- Uhaba wa malisho utapungua.
- Tatizo la Mifugo kuharibu mazao wakitafuta malisho litaepukika

Iwapo wananchi watashirikishwa kikamilifu katika mipango ya maendeleo:

- Serikali itaweka mipango mizuri inayotekelezeka na kukubalika na wananchi
- Tabia ya kuhamahama ovyo itapungua na hivyo kupunguza mwingiliano katika matumizi ya ardhi
- Mipango mizuri itawezesha ufugaji unaowiano na maeneo yaliyopo.

### 2.4.4 Wakulima wa wilaya za Mbeya

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 4: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wa wilaya za Mbeya**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Utoaji rushwa kwa wenye uwezo | 50 |
| 2. | Elimu duni ya kilimo na ufugaji | 35 |
| 3. | Wachungaji kutokuwa makini | 15 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Iwapo rushwa itakomeshwa:

- Jeuri ya wachungaji itakoma na pia
- Kutakuwepo na maelewano ya dhati uharibifu unapotokea na hivyo mahusiano baina ya wakulima na wafugaji kuwa imara.

Wakulima wa wilaya za Mbeya wanatazamia pia kuwa iwapo wakulima na wafugaji watatumia utaalamu katika uzalishaji:

- Wataepuka kilimo na ufugaji wa kuhamahama
- Watafuga kwa uwiano sahihi na maeneo yaliyopo
- Malisho yatakuwa ya kutosha
- Na hivyo kuepuka wakulima kulima maeneo ya malisho au mifugo kuharibu mazao
- Migogoro inayohitaji usuluhisho itapungua.

Iwapo wafugaji watakuwa na wachungaji makini:

- Uharibifu wa mazao kutokana na mifugo kuingia mashambani utapungua.

### 2.4.5 Washauri wa ugani na watafiti

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 5 Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa washauri wa ugani na watafiti**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Mfumo mbaya wa umilikaji wa ardhi | 29 |
| 2. | Mila na desturi potofu | 27 |
| 3. | Rushwa | 15 |
| 4. | Kutotenga maeneo ya kilimo na ufugaji | 10 |
| 5. | Ongezeko la watu na mifugo | 10 |
| 6. | Kutoshirikisha wananchi katika kupanga matumizi ya ardhi | 9 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Iwapo mfumo wa umilikaji ardhi utakuwa mzuri,

- Kwa kiasi kikubwa wafugaji watatambua umuhimu wa kuwa na idadi ya mifugo inayowiana na eneo
- Serikali haitaweza kufungua miradi katika maeneo ya wakulima na wafugaji.
- Mwanya au haja ya wakulima na wafugaji kuhamahama haitakuwepo.
- Hayo yataondoa tatizo la mifugo kuingiliana na mazao.

Aidha iwapo hapatakuwa na mila potofu baina ya wakulima na wafugaji

- Watatafuta na kutumia elimu bora katika uzalishaji
- Kasumba ya wafugaji kupenda sifa haitakuwepo.
- Hayo yatapelekea ufugaji na kilimo kuwiana na maeneo yaliyopo.

Iwapo rushwa itadhibitiwa

- Taasisi za haki na sheria zitatimiza wajibu wao kikamilifu
- Hivyo migogoro itapatiwa ufumbuzi muafaka na unaokubalika na pande zote.

Iwapo maeneo ya kilimo na mifugo yatetengwa kikamilifu

- Hakutakuwepo uharibifu wa mazao ya wakulima.

Pia iwapo ongezeko la watu na mifugo litadhibitiwa

- Haja ya kugombea ardhi itapungua.

Aidha kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika kupanga matumizi ya ardhi

- Kutaiwezesha serikali kuweka sheria zisizo gandamizi na zinazotekelezeka na hivyo kusaidia wakulima na wafugaji kutohitaji kuhamahama.

### 2.4.6 Wataalamu waandamizi wa wilaya

*iii. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

**Jedwali Na. 5 Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wataalamu waandamizi wa wilaya**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Mila na desturi potofu za wafugaji | 37 |
| 2. | Wakulima na wafugaji kutojua sheria | 30 |
| 3. | Viongozi kutoshirikisha wakulima na wafugaji katika kutoa maamuzi | 15 |
| 4. | Uwezo mdogo wa halmashauri za wilaya kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi | 13 |
| 5. | Vyombo vya haki vya kata na vujiji kutojua sheria | 5 |

*iv. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wafugaji wakiacha mila na desturi potofu

- Wataacha kuhamahama
- Wataachana na kasumba ya kuwa na mifugo mingi.
- Malisho ya kutosha yatakuwemo
- Mwingiliano katika matumizi ya ardhi utapungua.
- Mila na desturi potofu zitaachwa na hivyo itaboresha mahusiano katika jamii.
- Ushiriki wa jamii za wafugaji katika serikali za vijiji pia utaimarika.

Iwapo wakulima na wafugaji watakuwa na uelewa wa kutosha wa sheria

- nguvu ya rushwa haitakuwepo. Watoa rushwa na wapokeaji watashindwa kufanya hivyo kwa sababu wanajua kuwa mlalamikaji anajua namna ya kupata haki yake na lazima ataipata. Wanaolazimika kutoa rushwa kwa kutojua sheria hawatatoa kwa vile wanjua kuwa wanayo haki kisheria na hivyo hawahitaji kutoa rushwa iliwapate haki yao. Rushwa isipokuwepo mwingiliano katika

matumizi ya ardhi utapungua na pia waathirika wa migogoro watapata suluhu zinazoridhisha.

Viongozi wakiwashirikisha kikamilifu wakulima na wafugaji katika kutoa maamuzi ya migogoro inapotokea, itasaidia kuimarisha mahusiano.

Halmashauri za wilaya zikiwa na uwezo wa kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi

- Uhamaji holela wa wafugaji na wakulima utadhibitiwa
- Mwingiliano wa wakulima na wafugaji katika matumizi ya ardhi utapungua.

Aidha vyombo vya kata na vijiji vikiwa na uelewa wa kutosha wa sheria

- Vitatekeleza kikamilifu sheria ya mipango miji na nchi katika ngazi ya kijiji na
- Mwingiliano katika matumizi ya ardhi utaepukika.

# 3 MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI, MIKAKATI YAKE NA WAHUSIKA KATIKA UTEKELEZAJI

Washiriki wa warsha waliona kati ya matatizo viini yote yaliyobainishwa yanayohitaji ufumbuzi wa haraka ni:

- Rushwa
- Umilikaji na mipango mibaya ya matumizi ya ardhi
- Elimu duni ya ufugaji na kilimo

Waliridhika kuwa utatuzi wa matatitizo hayo utaboresha kwa kiwango kikubwa mahusiano baina ya wakulima na wafugaji.

## *3.1 Utatuzi wa rushwa*

Warsha ilizingatia mazingira yafuatayo katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo la rushwa

i. Uelewa mdogo wa sheria baina ya wakulima na wafugaji unaowafanya walazimike kutoa rushwa kwa kudhani kuwa hakuna njia nyingine ya kuwapatia haki zao. Aidha wanaopokea rushwa wanakuwa na uhakika kuwa waliowapotezea haki zao hawataona haja ya kuzifuatilia.

ii. Uwezo mdogo wa walalamikaji kufuatilia haki zao kiasi cha kutoweza kumudu gharama za kufuatilia haki zao. Wapokeaji rushwa huwa na uhakika kuwa waliowapotezea kaki zao hawatamudu kuzifuatilia.

iii. Hofu ya kusimama mahakamani. Huwafanya walalamikaji kuogopa au kushindwa kutoa madai yao kikamilifu au walalamikiwa kuona kuwa kusimama mahakamani ni hukumu tayari dhidi yao.

iv. Urasimu wa vyombo vya sheria unaosababisha waathirika kutumia muda mwingi na fedha nyingi kufuatilia haki zao, hivyo kufanya watendaji kutumia mwanya huo kuwapotezea haki au kuwauzia haki waathirika kwa njia ya rushwa.
v. Tabia ya watendaji ya kusema njoo kesho isiyokwisha ili kushinikiza utoaji wa rushwa.
vi. Wasimamizi wa haki na sheria kutumia vitisho vya adhabu kali ili kushinikiza waaathirika kutoa rushwa
vii. Kipato duni kwa watendaji wa ngazi zote huwafanya watumie nafasi walizonazo kukidhi mahitaji yao.
viii. Tamaa ya kujilimbikizia mali. Huwafanya watendaji wapokea rushwa kudai rushwa bila kukoma ili wajipatie mali lukuki. Hali hii huwafanya watu wenye matatizo ya kisheria kuwa sehemu ya miradi yao ya kupatia kipato.
ix. Kuporomoka kwa maadili ya jamii. Rushwa (kutoa na kupokea) imekuwa ni sehemu ya maisha ya baadhi ya watu. Hawaoni haya kutoa au kupokea rushwa.

### 3.1.1 Ufumbuzi

i. Mlalamikaji kuwa na uwezo wa kufuatilia haki zake
ii. Mlalamikaji na mlalamikiwa kuwa na ufahamu wa kutosha wa haki na sheria
iii. Kuboresha kipato na masilahi ya watendaji
iv. Kuinua maadili ya jamii kuhusu mtazamo wa rushwa

### 3.1.2 Mikakati

i. Kuunda vikundi vya wakulima na wafugaji ili kujenga uwezo wa pamoja wa kutatua matatizo kisheria
ii. Elimu ya haki na sheria itolewe hadi vijijini
iii. Vijiji viwe na bajeti inayoonesha mapato na matumizi halisi yanayotarajiwa ili viweze kuweka mikakati ya kuwalipa watendaji wa vijiji.
iv. Watendaji wa vijiji wawe waajiriwa wa Halmashauri za wilaya mpaka hapo vijiji vitakapokuwa na uwezo wa kuwalipa watendaji wao
v. Yaundwe mabaraza ya kijamii ya kutatua migogoro na kukemea wanaotoa na kupokea rushwa katika jamii na kutatua matatizo kijamii bila kulazimika kwenda katika vyombo vya sheria ambavyo vimelalamikiwa kutotoa haki inavyostahili.

### 3.1.3 Watekelezaji na wajibu wao

i. Wakulima na wafugaji
- Waunde vikundi vya ushirikiano katika kutafuta haki na masilahi mengine ya kijamii. Wazee na watu wanaoheshimika katika jamii waungane na kuunda mabaraza ya kijamii.
- Watafute na kutumia utaalamu na elimu ya sheria.
- Wawajibike katika kulipa kodi za maendeleo ili serikali zao za vijiji ziwe na uwezo wa kusimamia sheria na haki zao kikamilifu.
- Wahoji na kuelewa namna kodi yao inavyotumiwa na serikali za vijiji na halmashauri za wilaya.
- Waepuke njia za mkato katika kumaliza mashauri yao.

ii. Wataalamu

- Watafiti wabuni mbinu muafaka zinazotekelezeka katika uundaji wa vikundi vya wakulima na wafugaji.
- Wabuni njia rahisi na fanisi ya kufikisha elimu ya sheria vijijini kwa walengwa.
- Watoe elimu juu ya umuhimu wa kulipa kodi na kuwawezesha wananchi kuhoji matumizi ya kodi yao.
- Kutoa elimu ya sheria kwa watendaji na elimu ya uandaaji wa bajeti za vijiji.
- Kutafiti zababu zilizosababisha kushuka kwa umuhimu wa mabaraza ya jadi na kubuni mbinu za kufufua mabaraza hayo.
- Wataalamu wa sheria wabuni njia fanisi na zisizo na ukiritimba katika kuamua mashauri ya kijamii mahakamani na hatua zote na rufaa zisiwe na gharama kubwa bila kuhitaji muda mwingi wa ufuatiliaji.

iii. Serikali

- Ipunguze urasimu wa kuandikisha vyama vya kijamii. Hatua zote ziishie wilayani. Iwezeshe wataalamu kutoa huduma ya elimu ya sheria katika jamii.
- Iwawezeshe wataalamu kubuni mbinu fanisi na zisizo na ukiritimba.
- Mapato kutoka vyanzo mbalimbali katika vijiji yatumike kutoa malipo na maslahi yanayostahili kwa watendaji wake.
- Vijiji na halmashauri zitengwe kulingana na uwezo wake kiuchumi katika kumudu gharama za utawala, ili kila halmashauri na kijiji kiweze kutoa masilahi bora kwa watendaji wake.
- Halmashauri za wilaya ziwaajiri watendaji wake (mwenyekiti na mtendaji wa kijiji).
- Halmashauri ziboreshe ukusanyaji wa kodi na mapato mengine.
- Halmashauri zioneshe manufaa ya kodi kwa walipaji ili walipaji wahamasike kulipa kodi bila kukwepa au kulazimishwa.

## *3.2 Utatuzi wa kuwezesha umilikaji na matumi zi sahihi ya ardhi*

### 3.2.1 Ufumbuzi

i. Kuwe na mipango ya kitaifa ya matumizi bora ya ardhi. Kila kipande cha ardhi nchini kieleweke matumizi yake. Kusiwepo na eneo wazi lisilojulikana matumizi yake ya wakati huo au ya baadaye. Maeneo ya akiba kwa ajili ya upanuzi wa kilimo, ufugaji au shughuli nyingine yaeleweke na utaratibu wa kuyatumia yanapohitajika ueleweke. Yawe na hadhi ya hifadhi ya taifa lakini kusiwepo ukiritimba inapohitajika kutumika kwa upanuzi wa shughuli iliyokusudiwa.

ii. Kila mkulima na mfugaji awe na eneo la kutosha kwa ajili ya shughuli yake anayoifanya.

iii. Kila mkulima au mfugaji amiliki kisheria ardhi anayotumia kwa shughuli yake.

iv. Wafugaji na wakulima waunde vikundi vitakavyo milikishwa ardhi kisheria ili waweze kumudu gharama zinazohitajika katika umilikishwaji wa ardhi. Wanavikundi wagawane na kumilikishana kijadi eneo wanalomiliki kisheria kama kikundi.

### 3.2.2 Mikakati

i. Tathmini ya maeneo yanayofaa kwa kilimo na yale yanayofaa kwa ufugaji ifanywe na yagawiwe kwa wakulima na wafugaji iliwayamiliki kisheria. Yanayobaki yahifadhiwe kwa upanuzi wa baadaye. Kama maeneo hayatoshelezi kulingana na mahitaji yalivyo hivi sasa basi serikali itathmini mahitaji ya upanuzi wa kilimo na ufugaji kutokana na ongezeko la watu ili eneo hilo la upanuzi litengwe. Eneo litakalobaki liwekewe kiwango maalumu cha ugawaji kukidhi eneo lililopo. Mfano mfugaji atapewa eneo la kutosha mifugo yake lakini lisizidi hekita 1000. Mkulima apewe eneo la kulima lakini lisilozidi hecta 500.

ii. Iundwe sheria inayozuia kuingilia maeneo yasiyotumika bila utaratibu maalumu wa upanuzi wa shughuli husika.

### 3.2.3 Watekelezaji na wajibu wao

i. Wakulima na wafugaji
- Wadai na washiriki katika zoezi la kumilikishwa kisheria ardhi wanayotumia.
- Waunde vikundi vya kumiliki ardhi kisheria na kusaidiana kuendeleza maeneo wanayomiliki mmoja mmoja.
- Wawajibike kuendeleza maeneo yao na kuzalisha kitalaamu kwa tija na uendelevu.
- Washirikiane na wataalamu kutoa takwimu halisi za mahitaji yao.

ii. Wataalamu
- Wabuni njia rahisi na fanisi ya kutathmini uwezo wa ardhi na mahitaji ya kilimo na ufugaji katika taifa.
- Watafiti mbinu bora na zinazokubalika kuboresha ufugaji na kilimo kwa tija na uendelevu.
- Wajenge uhusiano bora wa mawasiliano na wakulima na wafugaji ili wasiwaone wataalamu kama watoza kodi ya mifugo au mali zao na hivyo kuwakwepa wanapokwenda kuwahudumia.

iii. Serikali
- Iwe na takwimu sahihi za uwezo wa nchi na mahitaji kwa kilimo na ufugaji.
- Ihakikishe kuwa kila mkulima na mfugaji analima na kufuga katika eneo analolimiliki kisheria.
- Iunde na kutekeleza haraka sheria ya matumizi ya ardhi inayomtaka kila mkulima na mfugaji kufuga na kulima katika eneo lake analolimiliki.
- Halmashauri zisiwahusishe wataalamu wa kilimo na mifugo katika utozaji wa kodi.
- Ishirikishe wananchi katika hatua zote za upangaji wa mipango ya matumizi.

### 3.2.2 Mikakati

i. Tathmini ya maeneo yanayofaa kwa kilimo na yale yanayofaa kwa ufugaji ifanywe na yagawiwe kwa wakulima na wafugaji iliwayamiliki kisheria. Yanayobaki yahifadhiwe kwa upanuzi wa baadaye. Kama maeneo hayatoshelezi kulingana na mahitaji yalivyo hivi sasa basi serikali itathmini mahitaji ya upanuzi wa kilimo na ufugaji kutokana na ongezeko la watu ili eneo hilo la upanuzi litengwe. Eneo litakalobaki liwekewe kiwango maalumu cha ugawaji kukidhi eneo lililopo. Mfano mfugaji atapewa eneo la kutosha mifugo yake lakini lisizidi hekita 1000. Mkulima apewe eneo la kulima lakini lisilozidi hecta 500.

ii. Iundwe sheria inayozuia kuingilia maeneo yasiyotumika bila utaratibu maalumu wa upanuzi wa shughuli husika.

### 3.2.3 Watekelezaji na wajibu wao

i. Wakulima na wafugaji
- Wadai na washiriki katika zoezi la kumilikishwa kisheria ardhi wanayotumia.
- Waunde vikundi vya kumiliki ardhi kisheria na kusaidiana kuendeleza maeneo wanayomiliki mmoja mmoja.
- Wawajibike kuendeleza maeneo yao na kuzalisha kitalaamu kwa tija na uendelevu.
- Washirikiane na wataalamu kutoa takwimu halisi za mahitaji yao.

ii. Wataalamu
- Wabuni njia rahisi na fanisi ya kutathmini uwezo wa ardhi na mahitaji ya kilimo na ufugaji katika taifa.
- Watafiti mbinu bora na zinazokubalika kuboresha ufugaji na kilimo kwa tija na uendelevu.
- Wajenge uhusiano bora wa mawasiliano na wakulima na wafugaji ili wasiwaone wataalamu kama watoza kodi ya mifugo au mali zao na hivyo kuwakwepa wanapokwenda kuwahudumia.

iii. Serikali
- Iwe na takwimu sahihi za uwezo wa nchi na mahitaji kwa kilimo na ufugaji.
- Ihakikishe kuwa kila mkulima na mfugaji analima na kufuga katika eneo analolimiliki kisheria.
- Iunde na kutekeleza haraka sheria ya matumizi ya ardhi inayomtaka kila mkulima na mfugaji kufuga na kulima katika eneo lake analolimiliki.
- Halmashauri zisiwahusishe wataalamu wa kilimo na mifugo katika utozaji wa kodi.
- Ishirikishe wananchi katika hatua zote za upangaji wa mipango ya matumizi.

## *3.3 Elimu duni ya kilimo na ufugaji*

### 3.3.1 Ufumbuzi

i. Wakulima na wafugaji waweze kumudu gharama za pembejeo
ii. Wakulima na wafugaji wawe na kiwango cha kutosha cha elimu.
iii. Wataalamu wa ugani wawe wa kutosha
iv. Mbinu za ugani ziendane na wakati na mazingira

### 3.3.2 Mikakati

i. Kupunguza gharama za pembejeo
ii. Kuondoa fursa ya wakulima kuhamahama kiholela
iii. Kuinua ufanisi wa elimu ya msingi vijijini
iv. Kuongeza idadi ya wataalamu wa ugani vijijini

### 3.3.3 Watekelezaji na wajibu wao

i. Wakulima na wafugaji
- Wathamini elimu ya msingi na washiriki katika kuboresha huduma ya elimu vijijini.

ii. Wataalamu
- Watumie mbinu sahihi na muafaka kulingana na mazingira na wakati
- Watoe ushauri unaotekelezeka na kukubalika kijamii

iii. Serikali
- Itoe ruzuku katika pembejeo za kilimo na ufugaji
- Iboreshe mazingira ya kazi kwa wataalamu wa ugani vijijini
- Iunde sera nzuri za masoko ya mazao ya wakulima ili kuinua kipato na tija katika uzalishaji
- Idhibiti ubora wa pembejeo ili wakulima na wafugaji wasikatishwe tamaa kwa kutumia pembejeo zisizo na ubora unaostahili
- Serikali za vijiji na Halmashauri za wilaya ziepuke kuwatumia wataalmu wa ugani katika ukusanyaji wa kodi ili wakubalike na kuaminiwa na jamii wanazozihudumia
- Iharakishe utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kama ilivyopendekezwa awali ili kuondoa mwanya wa wakulima na wafugaji kuhamahama holela.

# 4 HITIMISHO

## *4.1 Tamko la warsha*

Warsha ilitamka kuwa taarifa za kazi za warsha hii iwafikie watendaji wakuu wa Wizara za Kilimo, Maji na Mifugo, na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali ichukue hatua za haraka na sahihi badala ya kungoja mapigano kutokea. Kwa kuwa

migogoro mingi baina ya wafugaji na wakulima ni juu ya matumizi ya ardhi basi Serikali ifanye jitihada za makusudi kusambaza vijitabu vya sheria ya ardhi kwa wananchi na kuwahamasisha kuielewa.

## *4.2 Kufunga*

Warsha ilifungwa rasmi na Dk. A Tarimo Afisa Kilimo na Mifugo Wilaya ya Songea. Mgeni rasmi alisema kuwa aliwashukuru washiriki kwa mchango wao wa mawazo na waandaaji kwa kuhakikisha kuwawezesha washiriki kikamilifu. Alisisitizia washiriki kuhakikisha kufikisha yale waliyoyapata katika warsha hiyo kwa waliowawakilisha na wataalamu kufanyia kazi kikamilifu matokeo ya warsha.

# Viambatanisho

## Kiambatisho Na. 1: Orodha ya washiriki


| No. | Jina | Jinsia | Anuani |
|---|---|---|---|
| | **Wakulima/wafugaji** | | |
| 1. | Esther Kilemile | ke | S.L.P 29, Chimala, Mbeya |
| 2. | Veneranda Kasukumpa | ke | S.L.P 82, Mpanda |
| 3. | Editha Kambimbaya | ke | C/o Editha M. Kasafu S.L.P 108 Mpanda |
| 4. | Bertha J. Chifupa | ke | S.L.P 4610, Mbalizi, Mbeya |
| 5. | Meleso S. Mwinyipembe | ke | Mapogollo, P/Bag Idodi Iringa (V). |
| 6. | Jimmy L. Kinyunyu | me | S.L.P 1066 Lyamkena,Makambako |
| 7. | Daudi Njugunya | me | S.L.P 79 Mbarali Mbeya |
| 8. | Richard Ngwale | me | S.L.P 59 Itembula, Iringa |
| 9. | Godwin Mwantapika | me | S.L.P 2109,Njelenje,Mbeya |
| 10. | Lastoni Simbayanje Mwango | me | S.L.P 740 Mshewe,Mbeya |
| 11. | Mathias Makambuya | me | S.L.P 118 Mkwajuni Chunya Mbeya |
| 12. | Keneth Nicolas Mbonje | me | S.L.P 18 Mkwajuni Chunya |
| 13. | Daudi Muli | me | S.L.P 83, Ikoga Rujewa |
| 14. | Elikana Malamla | me | S.L.P 64 Rujewa Mbarali |
| 15. | Serendu Maitey | me | S.L.P 511, Iringa |
| 16. | Leonard Rafael Chengula | me | P/b Makifu Idodi Iringa |
| 17. | Pascal Mbagulila | me | S.L.P 33, Isevya Mpanda |
| 18. | Philopo Tembo | me | S.L.P. 82 Mpanda |
| | **Wataalamu wa ugani** | | |
| 1. | Julia Sandone | Ke | S.L.P 82 Mpanda |
| 2. | Msemembo Moses | me | S.L.P 78 Mafinga, Iringa |
| 3. | George Melkior Hyera | me | S.L.P 253 Mbeya |
| 4. | Reward Kirumba | me | S.L.P 171 Idodi,Iringa |
| 5. | Wedar Masanja | me | S.L.P. 107 Chunya, Mbeya |
| | **Watafiti** | | |
| 1. | Noel L. Kanuya | me | S.L.P 3020, Morogoro |
| 2. | Zacharia J. Mkoga | me | S.L.P 400, Mbeya |
| 3. | Charles M.D. Mutagwamba | me | S.L.P 400 Mbeya |
| 4. | Philbert Kapinga | me | S.L.P 400 Mbeya |
| | | | |

## Kiambatanisho Namba 2: Kielelezo cha mfano hai wa ajali nyingi barabarani




## Kiambatanisho Namba 3: Michoro inayoonesha uhusiano wa matatizo, viini vyake na kipaumbele katika utatuzi wa kila kiini


### Kiambatanisho 3 A: Kikundi cha wakulima wa wilaya za mkoa wa Mbeya




## Kiambatanisho 3 B: Kikundi cha wakulima wa wilaya za mikoa ya Iringa na Rukwa




## Kiambatanisho 3 C: Kukundi cha wafugaji wa wilaya za mkoa wa Mbeya



**Kiambatanisho 3 D: Kikundi cha wafugaji wa wilaya za mikoa ya Iringa na Rukwa**



## Kiambatanisho 3 E: Kikundi cha wataalamu, watafiti na wataalamu wa ugani ( kilimo na mifugo)



## Kiambatanisho 3 F: Kikundi cha wataalamu waandamizi wa wilaya ya Mbarali

